

Kupata Chanjo ya COVID-19

Vaccinate WA

CovidVaccineWA.org

Kupigana na janga hili la tandavu kumeguwa ngumu, lakini sasa tuna chanjo za kutulinda dhidi ya COVID-19.



Chanjo zinatolewa bila malipo yoyote kwako.

Serikali ya muungano itagharamia gharama ya chanjo yako. Watoaji wanaweza kukutoza ada ya kukupatia chanjo, lakini bima ya afya huenda itaigharamia. Watoaji wataondoa ada hiyo iwapo huwezi kuimudu.



Uliza ni dozi ngapi unahitaji.

Kutegemea na chanjo unayopokea, unaweza kuhitaji kati ya dozi 1 na 3. Analia na mhudumu wako wa afya kuhusu idadi ya dozi ambayo wewe au mtoto wako mnaweza kuhitaji. Wewe au mtoto wako mnaweza pia kuhitaji dozi ya busta miezi 2-6 baada ya kukamilisha misururu ya msingi.



Chanjo hizo ni salama na zinafaa.

Chanjo zote ama zimeidhinishwa kamili kwa ajili ya matumizi ya na U.S. Food and Drug Administration (FDA, Usimamizi wa Chakula na Dawa Marekani)—kumaanisha kuwa FDA haikupata wasiwasi wowote wa usalama.



Mtu yeyote aliye na miezi 6 na zaidi anaweza kupokea chanjo.

Chanjo ya COVID-19 inapatikana kwa watu wote walio na umri wa miezi 6 na zaidi. Tembelea [VaccineLocator.doh.wa.gov](https://www.vaccineLocator.doh.wa.gov) ili kupata na kuratibu miadi. Unaweza pia kupiga 1-800-525-0127, kisha kubofya #. Kwa huduma za ukalimani, sema lugha yako simu itakapojibiwa.



Unaweza kuhisi madhara.

Kama chanjo nyingine za kawaida, unaweza kupata uvimbe katika mkono, homa, maumivu ya kichwa, au uchovu baada ya kupewa chanjo. Hizi ni dalili kuwa chanjo inafanya kazi.



Kuwa salama.

Baada ya kupata chanjo, vaa barakoa yako, kaa futi sita (mita mbili) mbali na wenzako, na kuwa na mikutano ya watu wachache.

Maswali? Tembelea: www.CovidVaccineWA.org

Kupata Chanjo ya COVID-19

Ni chanjo gani zinapatikana?

Kuna chanjo nne zinazopatikana - Pfizer, Moderna, Novavax, na Johnson & Johnson.

Kila dozi ilipewa idhini na FDA kwa matumizi ya dharura. Wataalamu wa matibabu kwenye Kamati ya Ushauri wa Matendo ya Chanjo na Kikundikazi cha Ukaguzi wa Usalama wa Kisayansi katika Majimbo ya Magharibi walithibitisha kuwa chanjo zilitimiza viwango vyetu vya usalama.

Ni nani anafaa kupata chanjo ya COVID-19?

Ni chaguo lako kupata chanjo hiyo. Ukiamua kuipata, unafaa kuambia mtoaji wako wa chanjo ikiwa:

- Una historia ya mizio mikali
- Una homa
- Una tatizo la kuvuja damu au unatumia dawa za kuzuia mgando wa damu.
- Una kingamaradhi iliyodhoofika au unatumia dawa ambayo inaathiri mfumo wa kingamaradhi
- Wewe ni mjamzito, unapanga kuwa mjamzito, au unanyonyesha
- Tayari umepokea chanjo nyingine ya COVID-19

Hufai kupata chanjo ikiwa umekuwa na mzio mkali kwa dozi iliyopita ya chanjo ya COVID-19 au kwa kiambato chochote katika chanjo hiyo.

Chanjo hizo zina kiambato amilifu, pamoja na mafuta, chumvi, na sukari ili kulinda chanjo na kuisaidia kufanya kazi vizuri kwa mwili.

Lazima uwe na angalau miezi 6 au zaidi ili kupata chanjo za Pfizer-BioNTech au Moderna, miaka 12 au zaidi ili kupata chanjo ya Novavax, na miaka 18 au zaidi ili kupata chanjo ya Johnson & Johnson.

Kuna madhara gani?

Ni kawaida kuwa na madhara siku moja au tatu baada ya kupata chanjo. Madhara ya kawaida ni uchovu, maumivu ya misuli, maumivu katika mkono wako uliodungwa sindano, homa, maumivu ya kichwa, maumivu ya viungo, baridi, kichefuchefu, au kutapika. Dalili zako zisipopotea, wasiliana na daktari wako au kituo cha afya.

Unafaa kusubiri dakika 15 hadi 30 kabla ya kuondoka kwenye kituo cha chanjo ili mtoaji wa chanjo yako aweze kukusaidia ikiwa una mzio au madhara mengine. Huku ukisubiri, unaweza kujisajili kwa v-safe ili kuripoti madhara yoyote na: v-safe.cdc.gov (katika Kiingereza pekee).

Wewe au mtoaji wa chanjo yako pia anaweza kuripoti madhara kwenye Mfumo wa Kuripoti Tukio Hatari ya Chanjo (VAERS):

vaers.hhs.gov/reportevent.html

Piga simu kwa 911 ikiwa una mzio baada ya kuondoka kwenye kliniki.

Dalili za mzio zinajumuisha: ugumu wa kupumua, kuvimba kwa uso wako na koo yako, mdundo wa haraka wa moyo, upele mbaya mwilini wako wote, kizunguzungu na udhaifu.

Nini hufanyika baada ya kupata chanjo?

Iwapo wewe au mtoto wako mlipokea dozi mbili au tatu za chanjo, weka miadi ya dozi zako zinazofuata.

Utahitaji kurudi tena baada ya wiki 3-8 ili kupokea dozi zako zinazofuata. Kwa maelezo zaidi kuhusu ratiba ya chanjo, tafadhali tembelea doh.wa.gov/covidbooster

Itachukua hadi wiki mbili baada ya kupokea dozi kamili ili kupata ulinzi kamili. Inapendekezwa pia kupata dozi ya kiongeza nguvu wiki mbili hadi sita ili kuboresha kinga yako.



DOH 348-782 December 2022 Swahili

Ili kuomba waraka huu katika muundo mwingine, piga simu 1-800-525-0127. Wateja ambao ni viziwi au wasio na uwezo wa kuzungumza, tafadhali piga simu 711 ([Washington Relay](https://www.washington.gov)) au tuma barua pepe civil.rights@doh.wa.gov.